

Utoaji wa zawadi kwa kubadilishana na kujamiiiana

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Kutoa zawadi kwa mtu kwa kubadilishana ili kujamiiiana ni unyanyasaji mbaya. Iwapo mpokeaji wa zawadi hajakubali kujamiiiana na unamlazimisha, mwanamume au mwanamke kujamiiiana hapo hiyo ni unyanyasaji na unamwonea kwa sababu jambo hilo la kujamiiiana lilikuwa halikubaliki kwa mtu yule. Hapa Tanzania kosa la namna hii hujulikana kama unyanyasaji/ unyonyaji wa ujinsia10 ambapo mtu hufikiria kutumia fedha, mali au msaada kwa mtoto au wazazi kwa kusudi la kumpata ili ajamiiane naye.

Uwe mwangalifu unapopewa zawadi, alama za juu shuleni, au kuajiriwa kwa ajili ya kubadilishana na ngono. Kila mara uliza na jaribu kuelewa kwa nini zawadi inatolewa kwako. Usikubali zawadi yoyote au pesa, kama unafikiri kuwa huyo mtu anayekupa hongo kama zawadi, anakutegemea wewe kujamiiiana naye kwa kubadilishana na hiyo zawadi aliyokupa. Ni jambo la majaribu kukubali zawadi au pesa, hasa pale unapohitaji, lakini fikiri hatari itakayokupata kwa kujamiiiana kama vile mimba usiyoitarajia, magonjwa yaenezwayo kwa njia ya kujamiiiana hata Virusi na Ukimwi.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25630>